**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**

**MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI**

# HOTUBA YA MKURUGENZI MKUU WA LATRA KATIKA UFUNGUZI WA MKUTANO WA WADAU KUJADILI MAPITIO YA NAULI ZA TEKSI MTANDAO, DAR ES SALAAM

**Tarehe:** 11 Oktoba 2022 **Mahala:** Ukumbi wa Mikutano-Arnaoutoglou

---

- **Mheshimiwa Amos Makalla, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na Mgeni Rasmi kwenye Mkutano huu wa Wadau wa Teksi Mtandao,**
- **Ndugu Wakuu wa Taasisi, Viongozi wa Serikali na Sekta Binafsi,**
- **Ndugu Kaimu Katibu Mtendaji wa LATRA CCC;**
- **Ndugu Wamiliki wa Vyombo vya Usafiri wa Umma;**
- **Ndugu Madereva wa Teksi Mtandao;**
- **Ndugu Wasafirishaji na Watoa Huduma ya Usafiri wa Umma;**
- **Ndugu Wanahabari;**
- **Kamati ya Maandalizi ya Mkutano huu na Wenyeji wetu**
- **Wageni waalika mabibi na mabwana, Itifaki imezingatiwa**

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Tanzania**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi**, Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima, afya na fursa ya kuweza kukutana hapa leo ili kupokea mapendekezo ya mapitio ya nauli za teksi mtandao kutoka kwa wamiliki/waendeshaji wa mifumo wa teksi hizo (Bolt na Uber), kupokea maoni ya wamiliki wa teksi hizo, madereva wa teksi mtandao, watumiaji wa huduma hizo (abiria) na wadau wengine na kisha kumpa fursa Mdhibiti wa Huduma hizo

(LATRA) kufanya tathmini ya mapendekezo hayo kwa kuzingatia taarifa iliyo wasilishwa na maoni ya wadau.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** Pili, natoa shukrani za kipekee kwako binafsi na kwa Ofisi yako kwa ujumla kwa kukubali ombi letu na kujumuika nasi katika shughuli hii muhimu ya kupokea maoni ya wadau wa teksi mtandao kutoka Dar es Salaam kwenda vituo vya nje ya Dar es Salaam, na hata nje ya Tanzania (Afrika Mashariki na Afrika).

Tunafahamu kwamba unayo majukumu mengi, makubwa na muhimu katika ratiba zako, lakini umeweza kutenga muda na kufika hapa ili kutimiza jukumu hili ambalo pia ni la maslahi makubwa kwa Mkoa wa Dar es Salaam, Wasafiri toka ndani na nje ya Tanzania wenye kutumia usafiri huu wafikapo Dar es Salaam na Taifa letu kwa ujumla. Hii ni bishara njema kwetu, wadau tuliopo hapa na Watanzania wote kwamba tupo pamoja na Serikali yetu kwenye hili.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** naomba pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa wadau wetu wote, na hasa waliopo hapa, kwa kukubali mwaliko wetu na kuhudhuria mkutano huu. Ninatambua kila mmoja wetu ana majukumu mazito ya kiofisi au hata ya binafsi lakini kwa kutambua umuhimu wa Mkutano huu wameacha shughuli zao ili kwa pamoja tuweze kushirikiana katika hili.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** LATRA ni Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Tanzania Bara) na majukumu yake makuu ni udhibiti wa huduma katika usafiri kwa njia ya barabara, reli na waya (cable transport). LATRA ilitokana na iliyokuwa SUMATRA, ambayo ilifutwa na kuundwa TASAC na LATRA. Pamoja na Sheria ya LATRA, Tunazingatia pia Sheria ya Leseni (1973) na ya Reli (2017).

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** Huduma za Teksi Mtandao zilianza kutolewa hapa Nchini kabla ya kuwepo kwa Kanuni za Udhibiti wa usafiri huo. Aidha, baada ya kuanza kutumika rasmi kwa Kanuni za udhibiti wa usafiri huu, Mamlaka iliitisha kikao cha wadau kilichofanyika tarehe 21 Desemba, 2021, ili kupokea maoni na mapendekezo ya nauli za teksi mtandao. Kikao hicho kilifanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam. Wadau wa teksi mtandao walipewa nafasi ya kutoa maoni na mapendekezo yao kuhusu gharama za uendeshaji wa huduma hiyo. Utaratibu huu wa kushirikisha wadau ni kwa mujibu wa Kifungu cha 21 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura 413. Katika kikao hicho wamiliki wa magari, madereva, wananchi wanaotumia usafiri huo pamoja na wadau wengine kama Baraza la Watumiaji wa Huduma zinazodhibiwa na LATRA (LATRA-CCC) na Chama cha Kutetea Abiria (CHAKUA) walitoa maoni na mapendekezo yao kuhusu nauli pendekezwa. Hata hivyo, katika kikao hicho, kampuni za Bolt na Uber hawakuwasilisha mapendekezo yoyote kuhusu gharama za uendeshaji.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** Kwa mujibu wa Kifungu cha 19 (3) cha Sheria Sura 413, baada ya kuzingatia maoni ya wadau, Mamlaka ilitangaza Nauli Elekezi za teksi mtandao kwa Tangazo Na. LATRA/01/2022 la tarehe 14/3/2022 ambalo lilitolewa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 8/4/2022 kwa Tangazo Na. 1369 ambalo liliainisha viwango vya nauli ya teksi mtandao kama ifuatavyo:

a) Nauli kikomo ya teksi TZS 900 kwa kilometa;
b) Nauli kikomo ya teksi kwa dakika TZS 100;
c) Kiwango kikomo cha nauli kwa safari fupi ni TZS 3,000; na
d) Kamisheni15%.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 26 na 27 cha Sheria ya LATRA, Sura 413 upande wowote ambao hauridhishwi na maamuzi ya LATRA unatakiwa kukata

rufaa kwa Jopo la Mapitio (Review Pannel) inayoratibiwa na Mamlaka au kupeleka malalamiko kwenye Baraza la Ushindani (Fair Competition Tribunal (FCT)) kwa kuzingatia kifungu cha 33(6) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413.

Hata hivyo, pamoja na kuzishauri kampuni hizo, hakuna aliyeleta maombi rasmi kwa Mamlaka kufanya mapitio ya nauli elekezi, isipokuwa kampuni ya Uber (T) Limited Uber ilifikisha suala hili kwenye Baraza la Ushindani (FCT) na kusajiliwa kama **Rufani Na. 9 ya Mwaka 2022 kati ya Uber Tanzania na LATRA**. Hata hivyo, Uber waliamua kutoa Rufani yao FCT tarehe 2 Septemba, 2022 na kurejea kwenye meza ya majadiliano na LATRA.

**Malalamiko yalikuwa haya:**

Makampuni ya Mifumo ya Teksi Mtandao - Kampuni za nje ya nchi ambazo zinajihusisha na biashara ya teksi mtandao (Bolt Operations OU na Uber BV) kupitia wawakilishi wao ambao ni Uber Tanzania Limited na Bolt (T) Limited walilalamikia Kamisheni ya 15% kuwa ni ndogo na haikidhi gharama za uendeshaji wakieleza:

a) Nauli zilizoidhinishwa zipo juu na kusababisha kupoteza wateja. Hivyo waliendelea kutoza nauli kati ya TZS 450 hadi TZS 650 kwa kilometa ili kuvutia wateja.

b) Kamisheni ya 15% ni ndogo na haina faida kwa kampuni zao.

c) Kufuatia malalamiko hayo, tarehe 13 Aprili, 2022 Kampuni ya Uber Tanzania Limited iliijulisha Mamlaka uamuzi wake wa kusimamisha

kwa muda huduma zake isipokuwa kwa usafiri wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu (Bajaji).

d) Kampuni ya Bolt (T) Limited imekuwa ikisisitiza kuwa itasimamisha huduma zake endapo commission ya asilimia 15 haitaongezwa. Aidha, kampuni hiyo imewasilisha maombi ya kuruhusiwa kutoza booking fee ya asilimia 10 ili kufidia hasara

Makampuni ya ndani ya Little Tanzania Limited, Proin Promotion Limited (Paisha) na Globcab Company Limited (Ping) yalianza kwa kutekeleza Tangazo la Tozo la Mamlaka. Hata hivyo, makampuni hayo yalilalamikia makampuni ya Bolt na Uber kutoza viwango vya chini na kuwafanya wakose wateja.

Majadiliano ya malalamiko yao yakisikilizwa kupitia vikao na vilivyojumuisha ilijumuisha wajumbe kutoka Wizara na Taasisi za Serikali ambazo zina majukumu tofauti katika kuwezesha na kudhibiti usafiri wa kukodi wa teksi mtandao. Wizara zilizoshiriki ni pamoja na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (WUU), Wizara ya Fedha na Mipango (Financial Intelligence Unit), Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji (WVBU), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Bolt waliendelea kutoa huduma wakati majadiliano yakiendelea hadi tarehe 10 Agosti 2022 walipotangaza kupunguza utoaji wa huduma zao Tanzania na kuzisitisha ilipofika tarehe 17 Agosti 2022.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** wakati wa utekelezaji wa nauli za teksi mtandao, Mamlaka kwa nyakati tofauti, ilipokea malalamiko kutoka kwa wadau hawa (Bolt na Uber) lakini pia kutoka kwa madereva wa teksi mtandao kupitia chama chao – Tanzania Online Drivers Association (TODA). Malalamiko yao yalikuwa:

a) Kampuni za Uber Tanzania Limited na Bolt (T) Limited kuendelea kutoza nauli chini ya viwango elekezi visivyo na tija na hatimaye kushindwa kulipia gharama za uendeshaji ikiwa ni pamoja na mikopo ya benki waliyopewa kwa ajili ya kununua magari.

b) Kuendelea kukatwa fedha zao kwa ajili ya kugharamia punguzo la bei ambalo hutolewa na wamiliki wa mifumo katika kuvutia wateja (promotion) ambalo hufanywa na Uber Tanzania Limited na Bolt (T) Limited.

c) Viwango vya nauli visivyoeleweka kinyume na utaratibu uliowekwa na Mamlaka. Kampuni hizi zililalamikiwa kubadilisha viwango vya nauli katika masaa tofauti ndani ya siku moja na kusababisha hasara kwa madereva.

d) Kushindwa kufanya kazi na makampuni ya teksi mtandao ya ndani (local companies) ambayo yamekuwa yakitoza nauli elekezi tofauti na kampuni za Uber Tanzania Limited na Bolt (T) Limited kwa sababu wateja wanataka huduma nafuu.

e) Kutoridhishwa na kiwango cha TZS 900 kwa kilometer kuwa kiwango cha juu cha nauli (Price Cap) na badala yake kuomba kiwe kiwango cha chini (minimum rate). Hali hiyo ilipelekea mnamo tarehe 19 Aprili, 2022

madereva kuvamia ofisi za Mamlaka  na kufunga barabara kwa saa kadhaa ili kushinikiza Bolt na Uber wasishushe nauli kupita kiasi

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** Mamlaka ilifanya vikao na TODA (05/09/2022), Bolt (07/09/2022) na Uber (08/09/2022) ili kuwasikiliza na kuona kuna umuhimu wa kuwapa nafasi ya kuwasilisha mapendekezo yao mbele ya wadau ili yajadiliwe na LATRA iweze kupata maoni na kufanya maamuzi.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** Kwa Mujibu wa Kifungu cha 19 cha Sheria ya LATRA, Sura ya 413 na Kanuni za Tozo (The Land Transport Regulatory Authority (Tariff) Regulations) za Mwaka 2020, LATRA ina jukumu la kupanga na kufanya mapitio ya nauli ya huduma zinazodhibitiwa katika usafiri wa ardhini (barabara, reli na waya) kwa kuzingatia gharama za utoaji wa huduma hizo; kuleta ushindani wenye mvuto kwenye soko; ulinganisho wa kimataifa (international benchmarks) kwenye nauli, gharama na mrejesho wa mtaji (return on investments), athari ya kifedha; na mahitaji ya wateja/abiria na wawekezaji.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** ili LATRA iweze kupanga nauli, mtoa huduma anayedhibitiwa (regulated service provider) anapaswa kuwasilisha maombi kwa LATRA. Baada ya kupokea maombi, LATRA humpa mtoa huduma nafasi ya kuwasilisha mapendekezo yake kwa wadau na pia kuwapa fursa wadau kutoa maoni yao juu ya mapendekezo yatakayowasilishwa. Hivyo, LATRA ilipokea maombi ya Bolt na Uber ya kufanya mapitio ya nauli za teksi mtandao, na kwa mujibu wa taratibu, tunatoa fursa kwa waombaji kuwasilisha mapendekezo yao kwa wadau na kasha wadau watoe maoni dhidi ya mapendekezo yatakayowasilishwa.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** baada ya maelezo haya, napenda kukufahamisha kuwa Mkutano wetu wa leo utakuwa na sehemu kuu mbili.

1. tutawapa nafasi Bolt na Uber kuwasilisha mada yao ambapo watapaswa kuonesha uchambuzi uliowawezesha kufikia mapendekezo ya nauli waliyoyatoa, na
2. tutatoa nafasi kwa wadau kutoa maoni kuhusu kilichowasilishwa na Bolt na Uber na LATRA itayachukua na kwenda kuyafanyia tathmini.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** katika tathmini ya LATRA, Sheria inataka tuhakikishe kuwa mtoa huduma aweze kutoa na kuendelea kutoa huduma kwa ufanisi na walaji (watumiaji wa huduma) – Watanzania, wapate huduma bora za usafiri wanazoweza kuzifikia (affordable) na zenye kuzingatia thamani ya pesa wanazolipa. Aidha, jukumu hilo hilo linalenga kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora, salama na endelevu kwa upande wa mtoa huduma.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** baada ya kukamilisha zoezi la kupokea maoni ya wadau, Menejimenti ya LATRA itafanya tathmini na kuwasilisha mapendekezo kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA kwa maamuzi na mapendekezo ambayo yatawasilishwa kwa Mamlaka za Serikali (Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali). Baada ya idhini ya Mamlaka za Serikali, nauli zitatangazwa kwenye Gazeti la Serikali, na zitaanza kutumika siku 14 baada ya kutangazwa kwa mujibu wa Kanuni.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** yeyote ambaye hataridhishwa na maamuzi ya mdhibiti (LATRA) katika zoezi hili na maamuzi mengine yeyote ya kiudhibiti, atapaswa kuzingatia vifungu vya 26 hadi 28 vya Sheria ya LATRA pamoja na Kanuni za Tozo za LATRA za Mwaka 2020. Hii ni pamoja na kuwasilisha pingamizi au malalamiko ndani ya siku 14 tangu kutangazwa kwa nauli hizo.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** LATRA, inatambua kuwa si wadau wote wangeweza kufika hapa leo na kwamba taratibu zinaruhusu kupokea maoni kwa njia ya maandishi. Hivyo, tumeweka utaratibu wa kuendelea kupokea maoni kwa njia ya maandishi katika Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu, S.L.P. 3093, Dar es Salaam, iliyopo Jengo la Mamlaka, Barabara ya Nkrumah; Au Ofisi yetu mpya ya Makao Makuu Dodoma ambayo tunahamia mwezi huu, Eneo la NCC, Kiwanja Na 6, S. L. P. 1742, 41104 Tambukareli, Dodoma. Maoni ya wadau kwa njia ya maandishi yatufikie kabla ya **tarehe 26 Oktoba, 2022**. Pia, maoni hayo yanaweza wasilishwa kwa baruapepe ya info@latra.go.tz na dg@latra.go.tz

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi,** Baada ya kusema hayo, kwa heshima na taadhima naomba sasa nikukaribishe uongee na hadhara hii na kisha utekeleze jukumu kubwa la **kufungua mkutano wa kupokea maoni ya wadau kuhusu mapitio ya nauli za teksi mtandao.**

Asanteni kwa kunisikiliza

CPA Habibu J. S. Suluo

**Mkurugenzi Mkuu LATRA**

**11 Oktoba, 2022**